mwanzo mpya

# KUMEKUCHA

Tovuti: www.kumekucha.co.tz | ISSN 4562-9710 Toleo Na.Toleo 0010 IJUMAA JANUARI 31, 2025 / Bei Tsh 1,000 Ksh 100



# Wasira aikomalia Chadema

UK 2

>Aionya isithubutu kuleta vurugu, >Asema Ikulu wataiona kwenye runinga tu



## Rais Samia apiga marufuku wageni kufanya umachinga

## Dk.Biteko aongoza mazishi wanafunzi saba geita

UK 2



**Noti mpya** kuanza kesho UK 2

**CUF yapata Katibu** Mkuu mpya Mwanamke UK 2

**Rais Kagame asalimu amri**

**Lissu ajitosa** kumtetea Dk.Slaa UK 3

## NOTI MPYA KUANZA KESHO

Na Benny Mwaipaja,

GAVANA wa Benki Kuu ya Tanzania,Emanuel Tutuba amesema kuwa noti mpya za Tanzania zenye saini ya Waziri wa Fedha,Dk.Mwigulu Lameck Nchemba na yeye mwenyewe zitaingia kwenye mzunguko kuanzia kesho Jumamosi Februari Mosi.

Gavana Tutuba amesema,noti hizo zitatumika sambamba na noti zilizopo hivi sasa zenye mwonekano wa noti zinazotumika hivi sasa zilizotolewa mwaka 2010, ikiwemo alama za usalama,ukubwa,rangi na mengine,isipokuwa ina marekebisho kwenye saini ya Waziri wa Fedha na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania.

Gavana Tutuba amesema hayo wakati akimkabidhi,Dk.Nchemba, Noti kifani za shilingi elfu kumi, elfu Tano, Elfu Mbili na Shilingi Elfu moja, katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha,Jijini Dar es Salaam, kwa mujibu wa Sheria na Taratibu zinazosimamia masuala ya fedha nchini.

Kwa upande wake Waziri wa Fedha,Dk.Mwigulu Lameck Nchemba,alimshukuru, Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu jambo hilo kufanyika na kumpongeza Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, kwa kusimamia mchakato wa uchapaji wa Noti hizo kwa weledi na uadilifu mkubwa.

Dk.Nchemba aliridhia Noti hizo ziingizwe kwenye mzunguko na kuanza kutumika kama ilivyopangwa tarehe moja Februari mwaka huu

# Stephen wasira aikomalia chadeama

NA STANSLAUS THOBIAS, GEITA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Stephen Wasirra serikali haitakubaliana na azimio lolote litakalopitishwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA)lenye lengo la kuvunja amani,umoja na mshikamano wa taifa.

Wasira ameyasema hayo jana mjini Bunda alipohutubia wananchi katika mkutano uliotumika kuzindua sherehe za maadhimisho ya miaka 48 ya kuzaliwa kwa CCM kupitia mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Stendi ya zamani.

Alisema,amesikia chama hicho kikitangaza kwamba kinakwenda kujifungia halafu kije na jambo ambalo halijapata kushuhudiwa nchini, hivyo anatoa angalizo mapema kuwa jambo hilo ni lazima lifuate katiba, sheria, kanuni na miongozo ya nchi endapo halitazingatia hayo CCM haitakubaliana nalo.

“Wamesema wanajifungia halafu waje wafanye jambo ambalo halijapata kuonekana, nikasema ni jambo gani, mimi nikaona huko kujifungia ile ni honeymoon maana honeymoon simnaijua, watu wakishaoana wanajifungia mahali…ile ni honemoon.

“Tunawaambia tunawatakia heri kwenye fungate lao lakini tunawaambia lolote watakalotoka nalo kwenye honeymoon lazima lifuate sheria, wakija na honeymoon inavunja amani hatuwezi kuwaunga mkono.

“Amani sera ya msingi ya Chama chetu na nchi yetu, sisi ni tofauti na nchi nyingine za Afrika hatujapigana wenyewe kwa wenyewe wala hatujapata kupinduana kwa hiyo hatuwezi kuruhusu kikundi cha watu kivuruge amani na tunawaambia katika suala la amani hakuna msalie mtume, tutalinda amani ya Tanzania kswa gharama yoyote,” alisema.

Alisema,Tundu Lissu ameona ukweli na umuhimu wa uchaguzi ndio maana ameamua hawezi kugomea uchaguzi “namkaribisha sana katika uwanja wa mapambano maana hilo ndilo jambo la msingi kwamba tutagombea naye.”

Wasira alisema,ana hakika CCM itapata ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu kutokana na mambo makubwa yaliyofanyika katika utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi.

“Ataweka wagombea, ila tunachomwambia ni kwamba tumejipanga kushinda kwa kishindo,tutashindana naye kwenye udiwani,ubunge na Urais ambao wataishia kuuona kwenye runinga tu.

“Rais wetu ni mwenye upendo mkubwa ameanzisha sera inaitwa 4R moja ni maridhiano na sisi CCM ni Chama kinachopigania amani,sisi ni Chama kinachosimamia maendeleo, sisi ni Chama kinachopigania umoja wa watu wa Afrika, hizo ndizo sera zetu za msingi.

Alisema,CHADEMA imeshindwa kutumia fursa iliyotolewa na Rais Samia ya kukaa pamoja na kujadili mambo ya msingi yanayohusu mustakabali wa taifa.

"Rafiki zetu wale walikuja wakasema hali ni mbaya sana turidhiane, wakaleta ajenda wanasema tuwaruhusu waliokimbia warudi na kwamba watakuwa salama, walirudi na wako salama.

## DK.BITEKO - AONGOZA MAZISHI WANAFUNZI SABA GEITA

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Bukombe, Dk. Doto Biteko ameongoza waombolezaji kuaga miili ya wanafunzi saba wa Shule ya Sekondari Businda iliyopo wilayani Bukombe, Geita waliofariki kwa kupigwa na radi Januari 27, 2025.

Katika shughuli ya kuaga miili hiyo iliyofanyika jana Dk. Biteko amekabidhi ubani kwa wafiwa huku akiwataka kuwa wavumilivu hasa kipindi hiki cha majonzi.

Ametoa pole kwa wazazi, walezi ndugu wa watoto pamoja na wanafunzi wa Businda kwa kuondokewa na wapendwa wao na wanajamii wa Businda Sekondari kwa jitihada na utoaji wa huduma wakati wa tukio hilo.

Alisema,Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan baada ya kupokea taarifa za msiba huo mzito amekuwa akifuatilia kwa karibu na kutoa maelekezo kwa ajili ya kuzifariji familia za wafiwa, wana Bukombe na Taifa kufuatia kuondokewa na vijana waliokuwa katika safari ya kutafuta elimu.

“Rais Samia amegharamia msiba pamoja na kutoa ubani kwa kila familia za wafiwa pamoja na kugharamia usafirishaji wa miili ya wanafunzi wawili kwenda Chato, Geita na Karatu mkoani Arusha kwa mazishi,” amesema.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Bulangwa, Theodora Mushi amesema wanafunzi hao walipatwa na umauti wakiwa katika harakati za kusaka elimu.

Wanafunzi wanne kati yao walifariki papo hapo na wengine watatu walifariki wakati wakipatiwa matibabu katika hospitali na vituo mbalimbali vya afya.

## CUF YAPATA KATIBU MKUU MPYA MWANAMKE

NA HUSNA NASSORO

BARAZA Kuu la uongozi wa Chama Cha Wananchi CUF,limemchagua Bi,Husna Abdallah kuwa Katibu Mkuu wake wa kwanza mwanamke wa chama hicho.

Huko nyuma CUF iliwahi kuwa na Naibu Katibu Mkuu,Magdalena Sakaya lakini katika kuonesha kuleta mapinduzi ya kutambua uwezo wa mwanamke imemchagua Bi Husna kuwa Katibu Mkuu.

Katika medani za siasa hapa Tanzania, Bibi Husna anakuwa ndio Mwanamama wa Kwanza kushika nafasi hiyo lakini pia hii inaonyesha jinsi Chama Cha Wananchi (CUF)kilivyo na uwazi inapotokea mwanachama mwenye sifa anapotaka kugombea nafasi yoyote.Aidha Bi. Husna alishinda kwa kupata kura 19 wakati mpinzani wake ndugu Ali Abarani alipata kura 11.

## BENKI YA DUNIA YATOA MCHONGO AJIRA KWA VIJANA TANZANIA

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Benki ya Dunia (WB) Ajay Banga ametoa matumaini kwa vijana wa Kiafrika wakiwemo Watanzania, kujiandaa kuingia katika soko la ajira ikiwa ni sehemu ya mipango inayoendelea kukamilika ya taasisi hiyo.

Alisema,katika muongo ujao, Vijana milioni 360 wa Afrika watakuwa tayari kuingia kwenye soko la ajira, kipindi ambacho pia mfumo wa Afrika unatarajiwa kutoa ajira kwa vijana milioni 250.

Banga aliyasema hayo katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika jijini Dar es Salaam na kuongeza kuwa kipindi hicho pia kitawaacha vijana watatu kati ya watano, bila fursa ya kazi inayowapa kipato na heshima.



## LISSU AJITOSA KUMTETEA DK.SLAA

NA MWANDISHI WETU

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA)Wakili Tundu Lissu, ameongeza nguvu katika jopo la mawakili wanaomtetea mwanasiasa mkongwe nchini Dk.Wilborad Slaa,katika kesi inayomkabili ya kusambaza taarifa za uongo kupitia mtandao wa X.

Lissu jana aliungana na mawakili wa utetezi wa Dkt.Slaa wakiongozwa na Peter Madeleka,Hekima Mwasipu, Mwanaisha Mndeme,Edson Kilatu na Paul Kisabo katika Mahakama Kuu ya Tanzania ambayo ilitoa agizo kwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu,kushughulikia dhamana ya mwanasiasa huyo.

Dk.Slaa alikosa dhamana tangu alipopandishwa kizimbani Januari 10,2025 ambapo alisomewa shitaka la kusambaza taarifa za uongo kupitia mtandao wa X ambapo mawakili wake walilazimika kufungua shauri la mapitio ya kesi yake katika Mahakama Kuu akipinga mwenendo wa Mahakama ya Kisutu kuahirisha usikilizwaji wa suala la dhamana yake kutokana na maombi ya kupinga dhamana yake yaliyotolewa na Jamhuri.

Akitoa maagizo yake jana,Jaji wa Mahakama Kuu,Arnold Kirekiano,alisema,kwa kuwa kesi ya msingi iko Mahakama ya Kisutu ambayo ina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na kwa kuwa hoja ya uhalali wa mashtaka ilishatolewa Kisutu na inasikilizwa na kupangiwa uamuzi amesema si vyema Mahakama Kuu kuingilia kati. Hivyo Jaji Kirekiano ameelekeza Mahakama ya Kisutu itoe uamuzi ambao ilishauandaa.

Akizungumza mara baada ya kutolewa maagizo hayo na Mahakama Kuu,Mwenyekiti wa Chadema na Wakili wa Dkt. Wilbroad Slaa, Tundu Lissu alisema,amesikitishwa na kushikiliwa kwa muda mrefu mteja wake huyo ambaye ana umri wa miaka 76 bila kupewa dhamana huku akieleza kuwa ni uonevu.

"Hivi inawezekanaje kwa serikali hii, na mapolisi wake na waendesha mashtaka wake kumweka ndani muda wote huu mzee wa miaka 76,Mzee Slaa alivyo ni tishio kiasi gani? Kama sio kukandamiza watu bure,Hivi ndiyo vitu ambavyo tunatakiwa tuvipige vita, tutengeneze nchi mpya, tupate sheria mpya, Katiba mpya itakayohakikisha kwamba mambo haya ya uonevu wa aina hii hayatokei tena kwa Wananchi wetu"

# RAIS SAMIAAPIGA MARUFUKU WAGENI KUFANYA UMACHINGA

Na Husna Nasorro,

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Dk.Samia Suluhu Hassan,amepiga marufuku wafanyabiasha wa kigeni kujishughulisha na biashara za Kimachinga.

Rais Dk.Samia amepiga marufuku hiyo jana katika hafla ya chakula cha mchana pamoja na washiriki wa zoezi la utafutaji na uokozi wa ajali ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa eneo la Kariakoo ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa wakati alipotembelea eneo la ajali Novemba mwaka jana.

Alisema,haiwezani shughuli zinazotakiwa kufanywa na vijana wa Kitanzania zifanywe na raia wa kigeni jambo ambalo serikali haiwezi kukubaliana nalo ambapo alitaka Waziri wa Viwanda na Biashara kushughulikia jambo hilo kwa haraka.

Alisema,Serikali itaimarisha mifumo ya usimamizi wa maafa na kuhakikisha inakuwa na utayari wa kukabiliana na dharura wakati wote.

Aidha,Rais Dk.Samia ametumia hafla hiyo kuwashukuru wote waliojitolea katika

zoezi la utafutaji na uokozi na amerejea msisitizo wake kuwa taarifa ya Kamati ya Uchunguzi wa ajali ya jengo kuporomoka Kariakoo itawekwa wazi hivi karibuni.

"Jengine ambalo tumepata somo hapa ni usimamizi wa serikali wakati wa ujenzi na kuhakikisha viwango vya ujenzi vinafuatwa. Kwa wake walililoliona jengo ulikuwa unaona kabisa ni mchanga mwingi kuliko nondo na saruji kwenye lile jengo

"Dar es Salaam tuna mradi wa DMDP ambao kati ya fedha za DMDP tumejipanga kujenga Soko jingine kubwa na nzuri kama la Kariakoo maeneo ya Jangwani, kwahiyo ni maoni yetu kwamba baadhi ya Wafanyabishara, Wanangu Wamachinga tutawahamisha tuwapeleke kwenye Soko lile la Jangwani na wakafanye biashara zao kwa nafasi"

Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia ameridhia mwaliko wa Mwenyekiti wa

Wafanyabiashara wa Kariakoo kufanya ziara katika eneo hilo la biashara kwa lengo la kuzungumza na wafanyabiashara wa eneo hilo.

Akijibu mwaliko kutembelea Kariakoo, Rais Dk. Samia amesema atatumia ziara hiyo pia kuzindua ukarabati wa jengo la Soko Kuu la Kariakoo huku akirejea azma ya Serikali kulifanya soko la Kariakoo kufanya biashara kwa saa 24.

Kwa upande wake Waziri Mkuu,Kassim Majaliwa alimwambia Rais Dk.Samia kwamba ripoti ya uchunguzi wa kuporomoka kwa jengo hilo na ukaguzi wa kina wa majengo yaliyoko eneo la Kariakoo imekamilika.

"Mheshimiwa Rais ulinielekeza kuunda kamati maalum ya kufanya uchunguzi wa kuporomoka kwa jengo na kufanya ukaguzi wa kina wa majengo mengine yaliyoko kwenye eneo la Kariakoo

"Napenda kukufahamisha kuwa kamati hiyo, wajumbe wake wote wako hapa ndani na imehitimisha kazi yake na kwa sasa nakamilisha taratibu za kuiwasilisha kwako nikiwa pamoja na timu nyingine iliyoundwa kwa kadri itakavyokupendeza siku yoyote na wakati wowote tunaomba utupangie muda pamoja na kamati kwa ajili ya kufanya mawasilisho mbele yako.

## TANAPA waanza maandalizi safari za treni

Na Zainab Ally - Dar es Salaam.

MAKAMISHNA wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Viongozi Waandamizi wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)wameanza maandalizi ya safari maalum za treni kuelekea ndani ya Hifadhi ya Taifa Nyerere kwa ajili ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani inayoadhimishwa kila mwaka ifikapo Machi 8.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi na Maendeleo ya Biashara Jully Limo alisema,

Aidha, Kamishna Jully pia aliambatana na Makamishna wengine kutoka Kanda ya Mashariki, Ofisi Kiunganishi ya Dar es Salaam, pamoja na Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Nyerere - ACC Ephraimu Mwangomo ambaye atakuwa mwenyeji wa wageni hao watakapokuwa wakifanya utalii ndani ya hifadhi hiyo yenye vivutio vingi.

Ikumbukwe kuwa safari kama hizi zilifanyika pia mwaka jana 2024 ambapo zaidi ya wanawake 100 walitumia treni ya TAZARA, huku Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ikiingiza wanawake zaidi 1,000 Siku hiyo ya Machi 08, 2024.

## Rais Kagame asalimu amri

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Rwanda Paul Kagame,amesema amekubaliana na serikali ya Marekani ya kusitisha mapigano mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Katika mazungumzo hayo, Kagame hakuashiria kusalimu amri kufuatia wito wa kuondoa wanajeshi wa Rwanda na waasi wa M23 kwenye mji wa Goma.

Kwenye mazungumzo ya simu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Marco Rubio alimshinikiza Rais Kagame kusitisha mara moja mapigano huku akielezea wasiwasi wake baada ya waasi hao wanaoungwa mkono na Rwanda kuingia Goma.

Kagame aliandika kupitia ukurasa wa X kwamba, amekuwa na mazungumzo yenye tija na Rubio kuhusu umuhimu wa kuhakikisha mapigano yanasitishwa Mashariki mwa Congo na kushughulikia mara moja kiini cha migogoro.

Marekani kwa muda mrefu imeionya Rwanda kuhusiana na hatua yake ya kuwaunga mkono waasi wa M23.Hivi sasa waasi wa M23 wameingia ndani zaidi ya mji wa Goma na kuchukua udhibiti wa uwanja wa ndege.

salaam

# Unafahamu tatizo la msongo wa mawazo?

WIKI iliyopita tulizungumzia sehemu ya kwanza ya tatizo la msongo wa mawazo na ufumbuzi wake.Katika mfululizo wa makala hii tuliishia kuzungumzia sababu zinazosababisha msongo wa mawazo.Sababu namba mbili inayosababisha msongo wa mawazo:

2.MATATIZO YA KIFEDHA

Msongo wa mawazo unaweza kusababishwa na matatizo ya kifedha kwa sababu zifuatazo

Ukosefu wa ajira, kudaiwa fedha nyingi sana,kulipwa fedha kidogo sana kwenye ajira au kibarua, kufukuzwa kazi na biashara kuingiza fedha kidogo sana.

Matatizo mengine ni mwenza wako kuiba mali zako na kuziuza kisha akatokomea kusikojulikana, kufilisika, kufilisiwa, kuibiwa, kudhulumiwa, kutapeliwa, kuvamiwa na majambazi,majanga ya asili kama ukame, mafuriko, tetemeko, kimbunga na watu kukopa fedha zako nyingi lakini hawarudishi.

3.MATATIZO YA KIFAMILIA/MAHUSIANO

Msongo wa mawazo unaweza kusababishwa na matatizo ya kifamilia/mahusiano kwa vyanzo vifuatavyo:

MAHUSIANO

Vyanzo ni kumfumania mwenza wako, kusalitiwa, kugundua mwenza wako amezaa na mtu mwengine, kugundua mwenza wako ameathirika na ugonjwa usiokuwa na tiba kama ukimwi, kutelekezwa na ujauzito,mwenza wako kutoroka kwenda kwao mara kwa mara,

Mwenza wako kukufokea, kukutukana, kukudhalilisha hadharani, kukuita majina ya udhalilishaji,kutishia muachane mara kwa mara,kukunyima unyumba kila siku, kukupa kashfa za uongo za usaliti kila siku,kupigwa mara kwa mara, kuingiliwa kinguvu, kuingiliwa kinyume na maumbile.Mwenza wako

kukubambikia kesi mahakamani,mwenza wako kuvunja mahusiano ghafla, mwenza wako kukata mawasiliano ghafla.

FAMILIA

Ugomvi wa mara kwa mara wa wazazi wako,ugomvi wa ndugu zako wa damu na wazazi wako,kutengwa na familia yako,talaka au kutengana kwa wazazi wako,kuuguza mzazi au wazazi,mzazi kuwa mzee sana au mlemavu.

4.MATATIZO BINAFSI

Unaweza kusumbuliwa na msongo wa mawazo kwa sababu binafsi kama vile

#kujichukia kwa muonekano, kusumbuliwa na ulemavu wa kudumu , kuichukia kazi yako,kuichukia taaluma yako,hofu ya kukosolewa,hofu ya kufa,kuichukia familia yako,kumchukia mwenza wako lakini hajakukosea chochote,

Tishio la usalama wako,tishio la kufungwa gerezani,tishio la kufukuzwa kazi, kukosolewa mara kwa mara kuathirika na ulevi kupindukia, kucheza kamari, kuvuta bangi, kutumia dawa za kulevya,kutumia fedha nyingi sana bila kujizuia.

Nyingine ni kuathirika na kujichua (masterbation),kujiona mzee sana kabla ya umri,kuona umri unazidi kuongezeka bila kupiga hatua yoyote kiuchumi na kifamilia.Kugombana na watu wa karibu mara kwa mara bila sababu zozote za msingi.

5.KUMBUKUMBU ZENYE KUHUZUNISHA NA MALEZI YA UTOTONI

Unaweza kusumbuliwa na msongo wa mawazo kwa sababu za kumbukumbu mbaya zenye kuhuzunisha kama vile kutekwa nyara,kubakwa, kulawitiwa, vipigo,kupata ajali yenye kusababisha ulemavu wa kudumu,kifo cha ghafla cha mpendwa wako, kusababisha ajali au kifo cha mpendwa wako kwa uzembe.

Kunyang'anywa mali, kufungwa gerezani, kushuhudia mzazi wako anapigwa, kufokewa, kutukanwa,kubamizwa ukutani, kurushiwa mawe, kunyimwa chakula, kufukuzwa nyumbani, kulazwa chooni,kubakwa , kulawitiwa,kuuawa n.k.

Vilevile kumbukumbu zenye kuhuzunisha kama kupigwa, kufokewa, kutukanwa,kudhalilishwa, kunyimwa chakula, kutengwa, kubaguliwa,kufanyiwa uonevu mara kwa mara.

III.MADHARA YA MSONGO WA MAWAZO

Madhara ya msongo wa mawazo ni kuongezeka kwa matatizo ya kiafya, kupitia kipindi kigumu sana kifedha,kutumia dawa za kulevya, pombe kupindukia, kuvuta bangi, kufukuzwa kazi,kufanya uhalifu, kujidhuru au kuwadhuru watu wengine.

UFUMBUZI WAKE

Msongo wa mawazo unaweza kukabiliwa kwa njia zifuatazo

1.KUJUA CHANZO CHA TATIZO HUSIKA

Unaweza kukabiliana na msongo wa mawazo kwa kufahamu chanzo cha tatizo lako na viashiria vya tatizo hilo.Kabla ya kukabiliana na msongo wa mawazo unatakiwa kukabiliana na viashiria vya msongo wa mawazo ambapo ni kupata utulivu wa akili.

Njia za kupata utulivu wa akili ni kama vile mazoezi ya kupumua (Deep breathing exercises, Yawning, Belly breathing) maelezo yake yako kwenye makala za nyuma pamoja na ndani ya kitabu cha JINSI YA KUPONA MAUMIVU MAKALI SANA MOYONI

2.TENGANISHA MATATIZO SEHEMU MBILI

Sehemu ya kwanza kuna matatizo yapo nje ya uwezo ambao hauna uwezo wa kukabiliana nayo kwa mfano hauna uwezo wa kubadilisha tabia ya mtu mwengine,hauna uwezo wa kubadilisha historia yako,hauna uwezo wa kutawala maamuzi ya watu wengine.

Hauna uwezo wa kuzuia watu wengine kufanya makosa,hauna uwezo wa kuzuia wapendwa wako kuugua au kifo kwa sababu ni mambo ambayo yanatokea kwa watu wote ulimwenguni bila kujali juhudi na umakini.

Hauna uwezo wa kuzuia mwenza wako kusaliti ila unaweza kumsamehe au kumuacha kisha uanze upya kutafuta mwenza mwengine.Hauwezi kumridhisha kila mtu haijalishi utaongea nini au kufanya kitu gani.

Matatizo ambayo yapo nje ya uwezo hutumika kujenga uvumilivu, kujifunza kusamehe, kujifunza tabia za watu, kubadilisha malengo au njia za kufikia malengo yako,kujua nguvu zako na madhaifu yako.

Kujua matumizi ya fedha,kupata uzoefu wa kitu fulani,kujua sifa za marafiki,kujua sifa za mwenza sahihi,kujua namna ya kujitetea,kujua namna ya kukabiliana na watu wenye tabia tofauti na za kwako.

3.TUMIA MAUMIVU YAKO KAMA HAMASA

Kwa mfano ututoni ulipitia manyanyaso unaweza kuanzisha kampeni ya kupinga ukatili kwa watoto,kwa mfano ulipitia manyanyaso kazini unaamua kuwa mtetezi wa wafanyakazi wenye kunyanyaswa kazini,kwa mfano ulidhulumiwa mali zako unatumia fursa hiyo kujifunza sheria na unakuwa mtetezi wa wenye kudhulumiwa,

Kama ulipitia ubaguzi shuleni unajifunza kukabiliana na vitendo vya ubaguzi popote uendapo,kwa mfano ulipitia kipindi kigumu sana kifedha unachukua uamuzi wa kujikwamua kifedha,

Kama mwenza wako alikufanyia udhalilishaji kwa sababu alikuwa na fedha nyingi zaidi yako unaamua kujikwamua kifedha kwa maana yale maumivu makali sana moyoni yanakuwa hamasa ya mafanikio badala ya kutaka kutia huruma kwenye jamii.

4.ZINGATIA KWAMBA: MATATIZO HUTOKEA KWA WATU WOTE ULIMWENGUNI

Matatizo hayatakwisha ulimwenguni haijalishi utalia,utacheka,utakata tamaa matatizo yapo palepale.Matatizo hayatazami malengo yako, matatizo hayatazami kipato chako, matatizo hayatazami machozi yako, matatizo hayatazami wewe ni mchamungu au mshirikina, matatizo hayatazami wewe ni muaminifu au msaliti,

Matatizo hayatazami wewe ni mlemavu au upo na viungo kamili, matatizo hayatazami umri wako, matatizo hayatazami familia ambayo umetokea, matatizo hayatazami kiwango cha elimu yako, matatizo hayatazami kama ni mgonjwa au upo na afya.

Matatizo hayatazami muonekano wako, matatizo hayatazami kama huwa unasaidia sana watu au hauna msaada wowote katika jamii, matatizo hayatazami unaishi wapi.Matatizo ni kama mvua ikinyesha inanyesha tu haijalishi unaishi kwenye ghorofa au nyumba ya tope.Ukikata tamaa haiwezi kuzuia mvua kunyesha au kujua kuwaka,ukikasirika kwa hali ya maisha yako haiwezi kuzuia kitu chochote hapa ulimwenguni.

Kama tatizo lako ni kubwa zaidi tunaweza kuwasiliana kwa ajili ya Counselling session na ufafanuzi wa kilichoandikwa hapo juu na utaona mabadiliko na kujisikia nafuu ndani ya muda mfupi baada ya mazungumzo.(Counseling kwa njia ya simu gharama Tshs 30000 , kuonana uso kwa uso Tshs 40000.

Mawasiliano

***+255766862579***

***+255622414991***

***Imeandikwa na Psychologist Said Kasege.Temeke,Dar es***



# CONGO DRC INA UBAVU KUITEKETEZA M23?



KUHUSU mapigano yanayoendelea kule nchini Congo DRC zamani ikiitwa ZAIRE, niwaambie tu kwamba M23 sio lolote kama nchi zifuatazo zitaamua ziache kufadhili hao waasi ama nchi hizo zivamiwe kijeshi na nchi ambazo zinapinga udhaalimu unaoendelea kwa wananchi wa DRC.

Sikia,hakuna namna yeyote ambayo nchi ya Rwanda inaweza kujisafisha kwamba ina wafadhili M23 kwa sababu kuna namna anahisi wale wanaoitwa Watutsi wanakandamizwa na DRC wala Uganda kujihami kwamba kuna kundi lipo pale linaloendesha mikakati kuivamia Uganda.

Kwa kifupi sana Uganda sio nchi ngeni kwa kujifanya wanaweza kujimegea ardhi katika mataifa jirani; mwaka 1978 hadi 1979 walikutana na kitu cha moto kutoka Tanzania baada ya kujaribu kujimegea ardhi ya mkoa wa Kagera. Ingelikuwa tunaweza kufanya subira kama hizi za DRC ule ujinga ungeendelea hivyohivyo hadi leo.

Nakutoa tu tongotongo.

Unakumbuka DR. JP Magufuli alivyoamua kubadili mapori ya akiba yaliyopo Karagwe na kuyapandisha hadi kuwa hifadhi za taifa? Unazifahamu sababu zake? Unaifahamu Kimisi? Unaifahamu Ibanda? Unaifahamu historia ya Burigi Chato ilivyoanzishwa?

Sikia hii; Magufuli hakutaka kucheka na nyani; wakati Hayati Dr JP Magufuli anaingia madarakani alikuta Tanzania na Rwanda hatuko vizuri kimaelewano. Magufuli alimuita mara kadhaa Kagame waongee, wakaongea na wakaterejea kuongea kwa mara nyingine tena. Lakini mazungumzo yale walau yalipata muafaka mzuri na hatimaye tukabaki bila uhasama mkubwa; ikabaki matumizi ya akili kumkwepa mtu mgomvi.

Nilikuuliza kuhusu Kimisi Game reserve, Ibanda na Burigi- Chato? Haya mapori tengefu yalianza kuingiza "nyoka" kwa mgongo wa wafugaji kutoka Rwanda. Mapori yale yalianza kutumika kutengeneza wavamizi. Mwaka 2018 Magufuli aliyapandisha hadhi na kuwa hifadhi za taifa. Wajinga wachache walikejeli kwamba Magufuli anahamisha wanyama anapeleka kwao Chato. Ukweli ni kwamba ule ulikuwa mpango mkakati wa kujilinda kwa uvamizi wa kupangwa.

Kuyapandisha hadhi yale mapori tengefu ulikuwa mpango mkakati kuondoa wavamizi ndani ya vichaka kwa kigezo cha wafugaji.Kinachoigharimu DRC leo hii ni kukosa stability ya kuyaweka chini mapori yake kimkakati.


Mapori yanapokuwa hayana ulinzi wa kimakusudi unakaribisha "wahuni" ndani mwako. Zile chokochoko za pale Kibiti na maeneo jirani unaweza kuona kwamba ulikuwa mpango mkakati wa wahuni pia. Shukrani kwa jeshi letu lilisafisha magugu yote.

Nataka kusema nini? Ukifuatilia historia ya hii vita ya DRC na - Waasi wake utaelewa nimesema nini hapa.Waasi wote wametokana na watawala walioko madarakani. DRC iliwakaribisha waasi bila kutambua. Kwa kifupi miaka ijayo Rwanda inaweza kuwa tishio kwa mataifa jirani, ni nchi ambayo inapaswa kudhibitiwa ipasavyo kila inapojaribu kufanya majaribio ya kipuuzi.

Leo hii DRC ikitaka iwe salama haihitaji kusumbuana na M23; iingie front pale Rwanda moja kwa moja iifute kwenye ramani. Hapo amani itakuwepo ya kudumu.

Ukitaka kumdhibiti adui yako, dhibiti njia zake kwanza. Rwanda akichapika hawezi kutoa msaada kwa M23. Vivyo hivyo Uganda aonywe. Uwezo huo DRC inayo. Kama ni vifaa vya kivita inahitaji ipate ufadhili wa Urusi. Ni ka ushauri tu.

# Sababu ya nyani jike kupenda nyani dume wenye pua kubwa



BBC

NYANI wenye pua kubwa ni mojawapo ya nyani wanaotambulika zaidi duniani.Katika siku za nyuma, ilisemekana kwamba pua zao zilikuwa kubwa sana, walipaswa kuzishikilia kwa upande mmoja ili waweze kula, lakini hii si kweli. Wanakula vizuri tu.

Wanapatikana katika kisiwa cha Borneo Kusini-mashariki mwa Asia, nyani hawa wa Ulimwengu wa Kale ni wa kijamii na wanyenyekevu. Wanaishi katika makundi; Kundi la majike huwa na dume mkubwa, anayetawala na majike na watoto wao.

Huishi msituni kando ya vijito na mito, ambapo hutafuta matunda, mbegu na majani. Matunda ambayo hayajaiva hupendelewa kwani kiwango cha juu cha sukari katika matunda yaliyoiva kinaweza kusababisha matumbo yao ambayo tayari ni mazito kutanuka zaidi.

Nyani

Watoto wa tumbili aina ya proboscis huzaliwa wakiwa na nyuso za samawati angavu na manyoya meusi, ambayo hubadilika polepole na kuwa rangi ya watu wazima wanapokua.

Ndio nyani pekee wanaojulikana kurejesha chakula chao na kukitafuna mara mbili na kuwa na tumbo mithili ya ng'ombe lenye vizimba vingi. Bakteria wa Symbiotic wanaoishi kwenye chemba husaidia kuvunja na kuondoa sumu ya chakula chao ambacho ni kigumu kusagwa.

Kila kitu kuhusu nyani hawa ni kikubwa.Tumbo lao ni kubwa, linajumuisha hadi robo ya uzito wa mwili wao.Wana miguu na mikia mirefu. Wao ni wakubwa kimwili, madume wanaweza kuwa na uzito wa hadi 24kg (karibu 52lbs).

Na bila shaka,pua zao ni kubwa na maumbo makubwa,wanavyoonekana, kama wale wa wakoloni wa Uholanzi waliokwenda Borneo katika karne ya 19, na kuwafanya watu wa eneo la Malai kumpa jina la utani tumbili huyo 'Orang Belanda'.

Nyani jike aina ya proboscis hupenda nyani wenye pua kubwa, ambayo ni maalum madume na inakua na hadi urefu wa 17cm (6.5in), ni sifa iliyochaguliwa yenye kuvutia kingono. Majike wanapendelea madume wenye pua kubwa na sayansi husaidia kueleza kwa nini.

Uchunguzi unaonesha kwamba madume wenye pua kubwa wana miili na korodani kubwa, na kwamba ukubwa wa pua huathiri ubora wa sauti za madume. Pua zao zina ashiria ufanisi katika masuala ya uzazi na, kwa kuzingatia hii, madume wenye pua kubwa huwa na majike wengi zaidi katika himaya zao.

Tumbili dume hutumia pua zao kubwa kuinua sauti na kuvutia wenzi.

Cha ajabu, madume wenye pua kubwa pia huwa na meno madogo mithili ya mbwa. Hili ni jambo lisilotarajiwa kwa sababu madume wa aina nyingine za nyani mara nyingi hutumia meno kwa ajili ya kupigana na kujilinda.



# DONALD TRUMP AWAFUNGUE FIKRA VIONGOZI AFRIKA



NA ASKOFU KALIKAWE BAGONZA

HABARI ya mjini ni Rais Donald Trump.Maamuzi ya kirais anayoyafanya yamezua gumzo dunia nzima. Mara kusitisha misaada, mara kufuta ruzuku kwa shirika la afya duniani (WHO),mara kurejesha wazamiaji makwao.

Mara kufuta uraia wa kuzaliwa wa watoto wa wazamiaji, mara kutambua jinsia mbili tu - mke na mme, na kupitia sheria ya talaka inayompa mwanamke nusu ya mali ya mmewe. Yako mengi. Kichaa kashika rungu, msio na uwezo wa kukimbia kaeni ndani.

Hata hivyo niseme mawili hata kama hamtayapenda:

1.DONALD Trump amewapigia kengele viongozi wa nchi za Afrika na wananchi wao. Miaka 60 baada ya uhuru,haiingii akilini kuwa bado tunaitegemea Marekani itupatie fedha za kufanya chaguzi za kuwachagua wala rushwa na mafisadi wa Afrika.

Halafu akitusema kuwa tunaiba chaguzi, tubinue midomo kusema kuwa “tuko huru asituingilie”. Hela za kuchaguana,kuchimba vyoo,kununua kondomu,madawa ya ukimwi,vyandarua - katupa yeye.

Akihoji, tunajishebedua eti tuko huru. Sasa kamfurusha kichaa na virago vyake tulizeni mshono kieleweke. Namuunga mkono Trump. Wahuni na wasela wananiona mwenzao kwa kutumia lugha yao. Nawajua kondoo wangu, nao wananijua.

2.Kuchaguliwa kwa Trump kumefichua siri ya wamarekani. Kwa nje wanajifanya wana demokrasia na wanaopinga ubaguzi wa rangi. Lakini kwa ndani wanamuunga mkono Trump kuzibagaza nchi maskini.Trump ni kioo halisi cha Wamarekani. Waliomchagua wanafanana naye.Tunabaguliwa na wamarekani siyo Trump kwa sababu hakujichagua wala hakuiba kura.

Hivi sasa nchi karibu zote za umoja wa Ulaya zimetekwa na roho ya kibaguzi (Zhenophobia).Hitler na Stalin wamefufuka.Huku nje wanajifanya kusikitika lakini ni wao wanaovipigia kura vyama vyenye mlengo wa kulia.Ukweli usemwe hata kama unauma. Afrika safisheni nyumba yenu.Ngoja tupambane. na hali yetu huko Kongo.

# UNAFAHAMU ASILI YA MGOGORO WA RWANDA NA CONGO DRC?

USIKU wa Machi 16,1996 viongozi wa Rwanda, Uganda, Sudani Kusini na Ethiopia pamoja na kiongozi wa AFDL Laulent kabila walisaini "Makubaliano ya mkataba wa Lemera".

Mkataba huu ulikuwa na shabaha ya kuigawa nchi hiyo kubwa mikononi mwa Marekani kupitia usimamizi wa Rwanda, Uganda, Sudani kusini na Ethiopia, huku Kenya na Tanzania wakiwa ndio wenyeviti wa kuinjinia mkataba huo wa lemela.

Japo baadae Tanzania ilijitoa kuunga mkono kuigawanya Kongo baadala yake ikaunga mkono msimamo wa Laurent Kabila katika kukataa kuutekeleza mkataba wa lemela, ambao kupitia mkataba huo ilizalishwa operation maalum iliyoitwa "Operation Banyamrenge".

Operation hii ililenga kumuondosha madarakani Mobutu, kiongozi wa muda mrefu wa Kongo na kibaraka wa Marekani ambao mpaka kipindi hicho walikuwa tayari wamemchoka kutokana na mabadiliko ya siasa za dunia.

Katika Makubaliano hayo yalio fanywa kati ya Laurent Desire Kabila na mataifa hayo huku Kabila akiwa kama kiongozi wa chama cha "kuikomboa Kongo" aliyekuwa akitaka kuondosha utawala wa dikteta Mobutu Sese Seko alipewa masharti ambayo yalianishwa kwenye mkataba wa Lemera.

Ambapo moja ya masharti ilikuwa ni kishirikina na wapiganaji wa Kinyarwanda kutoka Rwanda, Uganda na watutsi walio kuwa na makazi mashariki mwa Kongo, na baadae ya mapigano atoe sehemu ya ardhi mashariki mwa Kongo kama shukrani kwa Rwanda na Uganda huku akiruhusu usalama wa taifa hilo kuwa mikononi mwao.

Makubaliano hayo yalifanyika kwenye vilima vya Lemera vilivyoko Kivu ya Kusini katika mji wa Uvira na kujulikana kwa jina hilo, la "mkataba wa lemera" makubaliano hayo yalitaka Kabila, baada ya kuwa rais wa Kongo, aruhusu mikoa miwili ya Kivu Kaskazini na Kusini kuwa makazi ya Wanyarwanda wa kabila la Kitutsi.

Laurent Desire Kabila alikuwa tayari amechoka Kwa takribani miaka 20 ya kupambana na utawala wa Mobutu Sese Seko hivyo aliona ni bora kukubali masharti yeyote yale ya mkataba ili tu aweze kumtoa



Mobutu madarakani.

Ukweli ni kwamba pamoja na mkataba huo lakini bado Laurent Kabila alikuwa na hesabu zake kichwani ambazo alizipania kuwa geuka baada ya ushindi wa kumfurusha Mobutu ikulu ya Palace de la ñational' iliyopo Kinshasa, na inadaiwa kuwa baadhi ya mikakati baada ya ushindi aliwashirikisha TISS (shirika la kijasusi la Tanzania) ili wampe baraka za kuwageuka Rwanda na Uganda.

Baada ya makataba huo kusainiwa, ukainjinia operation maalum iliyopewa jina la "Operation Banyamrenge" operation hii ilisukwa vyema mjini Kigali, Rwanda kwa kuundwa kikundi cha wapiganaji waliojiita "wapinzani wa dikiteta Mobutu."

Hawa walikuwa Wakongomani na Wanyarwanda kutoka Rwanda na wengine waliokuwa wakiishi mkoa wa Kivu Kusini, Mashariki mwa Kongo. Katika kundi hilo alikuwemo Mkongomani, Jenerali Andre Kisasi Ngando, askari mtaalam wa kusomea aliyefunzwa ukomando China, USSR na Cuba.

# MKUTANO WA NISHATI UMEIACHIA HESHIMA KUBWA TANZANIA



A HUSNA NASORRO

MKUTANO wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika umemalizika hivi karibuni jijini Dar es Salaam kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam huku mwenyeji wake Rais Dk.Samia Suluhu akiweka rekodi ya kipekee.

Takwimu zinaonesha jumla ya Wakuu wa nchi 23 za Afrika walihudhuria Mkutano huo hatua ambayo inamfanya Dk.Samia kuwa Rais wa kwanza aliyepokea idadi kubwa ya viongozi wa ngazi ya juu tangu ipate uhuru.

Mara ya mwisho Tanzania kupokea ugeni mkubwa wa wakuu wa nchi za Afrika ilikua mwaka 1999 wakati wa Kifo cha Baba wa Taifa,Hayati Julius Kambarage Nyerere lakini hivi karibuni ilikuwa mwaka 2019 wakati Wakuu wa Nchi 15 walipohudhuria

Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Nchi ambazo Wakuu wa Nchi zao wanashiriki Mkutano huo kutoka Algeria,Comoro, Liberia, Lesotho, Botswana, Kenya, Ghana, Gabon, Sierra Leone, Ethiopia, Sudan na Malawi.Nyingine ni Zambia, Somalia, Guine Bisau, Burundi, Mauritania, Kongo Brazzaville, Madagascar, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Libya, Nigeria, Djibouti na Gabon.

Makamu wa Rais watakaoshiriki ni kutoka Gambia na Benin,Mawaziri Wakuu kutoka Cote d'Ivoire, Uganda, São Tomé and Príncipe na Equatorial Guinea na Naibu Mawaziri Wakuu ni kutoka Eswatine na Namibia.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Madini,Doto Biteko,anasema,Tanzania imepata wenyeji wa Mkutano huo kutokana na juhudi za Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kuifungua nchi katika masuala ya Diplomasia lakini kivutio kingine ni kuwa kisiwa cha amani.

Anasema,pia waaandaji wa Mkutano huo Benki ya Dunia(WB)wameichagua Tanzania kutokana na kuwa nchi ya Afrika iliyo mstari wa mbele katika mpango wa kupeleka umeme vijijini.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud mkutano huo ni mwendelezo wa matunda ya diplomasia ya Tanzania ambapo Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kutangazika barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Tanzania inatarajia kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati baada ya Dk.Samia kuridhia ombi la Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Mhandisi Innocent Luoga,Mkutano huo utahusisha Wakuu wa Nchi 54 katika Bara la Afrika, MaRais wa WB, AfDB, Umoja wa Afrika, Mawaziri wa Fedha na Mawaziri Nishati.

Akielezea chimbuko la Mkutano huo, Mhandisi Luoga anasema takwimu zinaonesha kuwa, takribani Waafrika milioni 685 hawajafikiwa na huduma ya umeme hadi sasa kati ya Waafrika zaidi ya Bilioni 1.

Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo Afrika wamekuja na Mpango Mahsusi ujulikanao kama Mission 300 ambao umelenga kuharakisha upatikanaji wa umeme kwa Waafrika Milioni 300 ifikapo 2030.

Anaeleza kuwa, Mpango huo unahusisha nchi zote za Afrika ambapo nchi 14 zimechaguliwa kuanza utekelezaji wa Mpango wa Mission 300 na nchi nyingine zitafuata.Amezitaja nchi hizo kuwa ni Tanzania, Mali, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ivory Coast, Bukina Faso, Chad, Liberia, Madagascar, Malawi, Mauritania, Msumbiki, Niger, Nigeria na Zambia.


Tanzania imeingizwa katika Mpango huo kwa kuwa ni nchi mwenyeji wa Mkutano kwani imeshapiga hatua kubwa katika usambazaji wa umeme kwa wananchi.

Anaeleza kuwa kupitia Mpango Mahsusi wa Kitaifa wa M300 unaofadhiliwa na WB, AfDB na Wadau wengine wa Maendeleo, Tanzania itaweza kuunganishia umeme watanzania milioni 13.5 yaani karibu mara mbili ya uwezo wake katika kipindi hicho cha miaka mitano na hivyo kufanya ongezeko la wateja milioni 8.3.

Mwanadiplomasia namba Moja wa Tanzania na Rais Samia ameendelea kuonesha Nguvu yake ya ushawishi Duniani kwa kuwaleta viongozi wa Dunia kuja kushiriki. Ikumbukwe huu ni mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika ila viongozi wa Dunia pia watakuja Kwa ushawishi wa Rais Samia chini ya ajenda yake kuu ya Nishati safi Kwa Wanawake.



# UJUMBE MZITO WA DONALD TRUMP KWA AFRIKA



MUNGU amebariki nchi zenu kwa rasilimali nyingi,akili, na uwezo mkubwa.Ni wakati wa kuacha kusubiri mabadiliko kutoka nje na kuanza kuwajibisha viongozi wenu wala rushwa.Acheni kukimbilia mataifa ya kigeni na kuzurura mitaani huko mkitafuta fursa ambazo zinapaswa kuwepo nyumbani kwenu.

Kama Wamarekani wangelikubali ukandamizaji na kubaki kimya, hakungekuwepo na Marekani kama unavyoiona sasa.Kama Wafaransa wangekaa kimya mwaka 1775, hangekuwa na Ufaransa ya leo.Mapinduzi yanahitaji hatua, si unyonge.

Kwa nini mnaendelea kucheza siasa za kikabila huku viongozi wenu wakiiba utajiri wa mataifa yenu bila haya?Kwa nini mnategemea Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa dawa za msaada wakati mna wataalamu wa madawa na tiba katika nchi zenu?Nchi zenu zimebarikiwa kwa vipaji na maarifa ya kutengeneza suluhisho za ndani.

Daini mifumo bora ya afya. Acheni viongozi wenu wakimbilie nchi za nje kutibiwa huku hospitali zenu nyumbani zikitelekezwa bila hata huduma thabiti ilihali mshajitawala tangu miaka ya 1960's.

Kwa nini viongozi wenu wanapora rasilimali zenu ili kuishi maisha ya anasa huku barabara zenu zikiwa mbovu, shule hazina fedha za kutosha, na umeme haupo wa uhakika?Je,mnasubiri malaika waje kutatua matatizo haya?M/Mungu amewapa uwezo wa kuchukua hatua, basi chukueni hatua.

Mataifa yaliyoendelea yamepata mafanikio kupitia uwajibikaji, kazi ngumu, na kujitolea, siyo kwa kusubiri miujiza.Marekani ni ya Wamarekani.Ufaransa ni ya Wafaransa.Ni wakati wa ninyi kuwajibika kwa nchi zenu. Acheni kukimbilia nchi za kigeni ili kujifungua na kutafuta uraia wa moja kwa moja kwa watoto wenu. Sera hizo zimeondolewa. Rudi nyumbani na mjenge Taifa ambalo mtaweza kujivunia kuzaliwa huko kwenu.

Mapinduzi huanza na watu,kama mmechoka na uongozi mbovu, inukeni. Dai takwimu sahihi za idadi ya watu, uchaguzi wa haki, na mwisho wa wizi na ufisadi. Acheni kuruhusu wanasiasa wala rushwa na viongozi wa kidini kuwapumbaza kwa kusema ukandamizaji ni “mapenzi ya Mungu.

Kama Wafaransa waliweza kuungana dhidi ya majeshi na watawala wakandamizaji, nanyi mnaweza. Mabadiliko hayatakuja ikiwa mtakaa kimya na kinyonge. Kama mnataka umeme wa uhakika, barabara nzuri, na maisha bora, chukueni hatua. Acheni kukimbilia Marekani, Canada, au Ulaya kwa kile ambacho mnaweza kujijengea nyumbani.

Ujumbe ni rahisi,inukeni, ungana, na mchukue hatima ya maisha yenu mikononi mwenu. Hatima ya Afrika ipo mikononi mwenu. Iwafikie mioyoni na akilini mwenu, ni ninyi pekee mnaoweza kuunda Afrika mnayoitamani.

# MAAMUZI YA TRUMP YATUFUNGUE MACHO HARAKA

NA MWANDISHI WETU

UTU wetu na thamani yetu, ilishuka miaka mingi, baada ya kuukumbatia ulemavu wa kusaidiwa.Tukubaliane waafrica, kuna ujinga fulani tumeushikilia, tungekuwa watu wa kuendelea kupitia misaada, tungeshatoka hapa tulipo.

Ukweli ni kwamba, misaada mingi ya magharibi haijawasaidia walengwa wa misaada hiyo zaidi ya kuishia mifukoni mwa watu wachache.Nitamshangaa Prof.Anna Tibaijuka, kuulizia Ukimwi ulianzia wapi?.Ukimwi ulianzia Marekani,Kama ulianzia huko, ni kwa nini Umeua na kuteketeza waafrica wengi zaidi??.

Motive ya kutengeneza,hivi virusi ilikuwa ni nini?.

Ukiisoma, na kuielewa Sayansi ya Kirusi kinavyoingia,kuathiri Chembe hai ya kinga ambayo ni ( Commander in chief), inayotoa amri, kwa chembei kinga nyingine, Lazima ukubaliane nami kuwa, maarifa ya binadamu ya " Genetic engineering yalifanya kazi.Dunia ina mengi ya kushangaza, Ngoja tujadiri tutawasaidiaje ndugu zetu wanaohitaji dawa hizi.

1) Kwa waafrica wote hii ni agenda yetu sote.a) Tu mobilise Resources,zetu tuwe na ushirika na wenye kupenda ushirika nasi, tujenge viwanda vyetu vya madawa, hata ikibidi kuwapeleka wana wa kiume na wa kike wa kitanzania, Kenya na nchi nyingine kupata maarifa ya juu zaidi ya kinga mwili( immunology).

b) Kila nchi inaweza kubeba jukumu moja moja, wakati Kenya wana tengeneza chanjo, sisi tujenge viwanda vya ARV.

2) Tuweke nguvu kwenye kukinga zaidi.a) Panaweza kuwa na vipimo vya kucheck kabla watu hawajaingiliana.b) Tutengeneze viwanda vya kuzalisha Condom nyingi.

C) Mtu anposhtuka kayatimba, basi guest zote ziwe na dawa za kuzuia kirusi hicho kusambaa( Post exposure prophylaxis).

d) Ngono duniani kote baadhi ya maeneo imekuwa ni commodity, basi kuwe na Priority kwenye nchi za kusaidia makundi yaliyoathirika kiuchumi, wapewe mikopo nafuu( serving disadvantaged societies),Ili ku shift equilibrium ya biashara ya ngono, kuja kwenye biashara nyingine.

3) 1,2, hapo juu zinaweza ku apply kama long term plan,



short term plan ni kama hizi.a) Tupunguze matumizi.

Badala ya magari ya mil 600, tununue magari ya mil 60!, b) Tuwe na mfuko wa Taifa wa Ukimwi i) 10% ya mauzo ya kodi yaende kwenye mfuko huu.

ii)Tuhamasishe matumize ya Teleconference, badala ya kulazimisha watu kusafiri kwa kuchoma mafuta ya petrol kwa ma V8 ili tuwe na hela ya emergency kwa ajili ya mfuko huu, badala ya kuitumia kununulia mafuta ya magari.

iii) 7% ya mapato ya mashindano yote kwenye mpira iende kwenye mfuko wa Taifa wa Ukimwi.Ninajaribu kuonyesha tu kuwa, hili tatizo liko ndani ya uwezo wetu!, Trump kutunyima misaada, ni NIA njema, ya kutaka tushtuke, tutumie raslimali zetu kwa faida ya watu wetu na si vikundi vya watu.

TUKATAE ULEMAVU WA KUSAIDIWA.



# mchakato kuwarudisha mateka wa Israel nyumbani kutoka Gaza unavyofanyika

MARA baada ya maelezo kupokelewa, timu kutoka Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC) inaondoka kwa magari yenye nembo ya shirika la kibinadamu ili kuwachukua mateka huko Gaza.

Wanajeshi wa Israeli na wafanyakazi wa kitabibu pia wamekusanyika katika maeneo kadhaa tofauti, wakingojea kuwarudisha nyumbani.

Kuachiliwa kwa mateka, kunatazamwa kote ulimwenguni, kumekuja baada ya miezi kadhaa ya mazungumzo ya mvutano yenye lengo la kumaliza vita vilivyoanza tarehe 7 Oktoba 2023, wakati wapiganaji wa Hamas walipowaua takribani watu 1,200 nchini Israel na kuwateka nyara wengine 251.

Katika miezi 15 iliyofuata, zaidi ya Wapalestina 47,000 waliuawa huko Gaza, kulingana na wizara ya afya inayoendeshwa na Hamas, na wengi zaidi walipoteza makazi yao katika mashambulizi ya Israel.

Chini ya masharti ya mkataba wa kusitisha mapigano kati ya Israel na Hamas ulioanza 19 Januari,jumla ya mateka 33 wa Israel wanastahili kuachiliwa na kurejeshwa kwa familia zao wakati wa awamu ya kwanza, itakayodumu kwa wiki sita.

Kwa kubadilishana, mamia ya wafungwa wa Kipalestina katika jela za Israel wanaachiliwa huru.Ikiwa chochote kitaenda vibaya, inahatarisha mateka kubaki utumwani, na vita kutawala."Hii ni zaidi ya kuendesha gari," anasema msemaji wa ICRC Sarah Davies.

"Operesheni hizi zinaweza kuonekana rahisi, lakini kwa kweli ni ngumu sana na zinahitaji hatua kali za usalama ili kupunguza hatari kwa wale wanaohusika."

ICRC, ambayo hufanya kazi kama mpatanishi asiyeegemea upande wowote katika makabidhiano, hukusanya timu ya wataalamu, ambao baadhi yao wamehusika katika shughuli kama hizo hapo awali, ingawa hii ni changamoto zaidi.

Je, uokoaji wa mateka wa Israel huko Gaza ulifanyikaje?

Kuna baadhi ya maelezo ambayo kundi hilo haliwezi kuzungumzia hadharani kwa sababu ya wasiwasi kwamba linaweza kuhatarisha usalama wa operesheni hiyo.

Bi Davies anasema kupanga ni muhimu ili kuhakikisha kuwa mabadilishano yanakwenda sawa.

Wamepanga njia mbadala za kufikia maeneo tofauti huko Gaza, wakijua kwamba "njia salama inaweza kubadilika" wakati wowote.

Miongoni mwa mahangaiko yao makubwa ni hatari zinazoletwa na silaha zisizolipuka, miundombinu iliyoharibiwa, na umati mkubwa wa watu wenye "hisia zilizoongezeka".

"Timu zetu hujiandaa na kupanga matukio mengi iwezekanavyo," anasema."Jambo muhimu zaidi kwetu ni kuweza kumrudisha nyumbani akiwa salama mtu yeyote aliyekabidhiwa chini ya uangalizi wetu."Lakini haiwezekani kupanga kwa kila kitu.

"Kutokana na uzoefu wa awali, hapa na katika maeneo mengine duniani kote, tunajua kwamba vifaa na maelezo ya mwisho yanaweza kubadilika wakati wowote, hata wakati wa operesheni yenyewe," anasema Bi Davies.

Wafanyakazi wa matibabu na wanaoitwa wataalamu wa uchafuzi wa silaha, waliofunzwa kutambua mabaki ya vita vya kulipuka, husafiri na timu.

Wakati wa operesheni, wawakilishi wa ICRC pia wanawasiliana mara kwa mara na maafisa wa Israeli na Hamas, pamoja na wapatanishi.Umati wa watu ulikusanyika katika Jiji la Gaza kwa ajili ya kuachiliwa kwa mateka watatu wa Israel.



# Nini kitakachofuata baada ya Mali,Niger na Burkina Faso kujiondoa Ecowas?

NCHI tatu zilizo chini ya utawala wa kijeshi zimeondoka rasmi katika kanda ya Afrika Magharibi Ecowas, baada ya zaidi ya mwaka mmoja wa mvutano wa kidiplomasia.Kujiondoa kwa Mali, Burkina Faso na Niger ni pigo kubwa kwa Ecowas, ambayo ina umri wa miaka 50 ikichukuliwa kuwa kundi muhimu zaidi la kikanda barani Afrika.

Mgawanyiko huo ulizuka baada ya nchi hizo tatu zinazoondoka kukataa madai ya Ecowas kurejesha utawala wa kidiplomasia.Siku ya Jumatano Ecowas ilisema itaweka "milango wazi" kwa Mali, Burkina Faso na Niger, ingawa wameendeleza kambi yao wenyewe, Muungano wa Nchi za Sahel (AES kwa kifupi katika lugha ya Kifaransa).

Ecowas ni nini?

Ecowas - ambayo inawakilisha Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi - ilianzishwa mwaka 1975 katika jitihada za kuboresha ushirikiano wa kiuchumi na kisiasa katika eneo la Afrika Magharibi.Kabla ya maamuzi ya Jumatano, kambi hiyo ilikuwa na wanachama 15, yakiwemo mataifa kama Nigeria, Ghana, Ivory Coast na Senegal.

Raia wa nchi zote za Ecowas kwa sasa wana haki ya kuishi na kufanya kazi katika nchi zote wanachama, kadhalika bidhaa kuweza kuzunguka kwa uhuru.

Kwanini Mali, Niger na Burkina Faso zimejiondoa?

Uhusiano kati ya Ecowas na nchi tatu za Sahel umekuwa wa wasiwasi tangu jeshi lilipochukua mamlaka nchini Niger mwaka 2023, Burkina Faso mwaka 2022 na Mali mwaka 2020.

Baada ya mapinduzi ya Niger, Ecowas iliweka vikwazo vinavyodhoofisha nchi hiyo, kama vile kufungwa kwa mipaka, kufungwa kwa safari za ndege zote za kibiashara na kufungiwa kwa mali za benki kuu.Ecowas pia ilitishia kupeleka vikosi vyake nchini Niger ili kurejesha utawala wa kidemokrasia.

Lakini uamuzi huu mgumu uliimarisha tu azimio la mataifa hayo matatu yanayotawaliwa kijeshi.Mali na Burkina Faso zilikosoa vikwazo vya "kikatili" vya Ecowas na kuapa kuilinda Niger ikiwa umoja huo utaingilia kijeshi.

Baada ya kusimamishwa na Ecowas, mataifa hayo matatu yalijibu kwa kutoa notisi Januari iliyopita kwamba wangejiondoa katika kipindi cha mwaka mmoja, wakitimiza ratiba iliyowekwa na jumuiya hiyo kwa mataifa ambayo yanaamua kujiondoa.

Mazungumzo kati ya Ecowas na mataifa hayo yanayotawaliwa kijeshi yamefanyika tangu wakati huo - lakini yameshindwa kubadili msimamo huo.Nchi hizo tatu zinaishutumu Ecowas kwa kuwa karibu sana na madola ya Magharibi na badala yake zimeegemea upande wa Urusi.

Je, kujiondoa huko kutaathiri vipi nchi hizo tatu?

Kwa mujibu wa nchi zinazojiondoa, sasa zitapata uhuru mkubwa zaidi na pia uhuru kutoka kwa jeshi ambalo lina ajenda ya kigeni.

Lakini wachambuzi wanasema Niger, Mali na Burkina Faso huenda zikatatizika nje ya jumuiya hiyo - hizi ni nchi maskini na zisizo na bahari ambazo uchumi wake unategemea majirani zao wa Afrika Magharibi.

Wakati Ecowas inafanyia kazi masharti ya uhusiano wake wa siku za usoni na nchi hizo tatu, inasema itaendelea kutambua hati za kusafiria na vitambulisho vyote vyenye nembo ya Ecowas inayotumiwa na raia kutoka Mali, Niger na Burkina Faso.

Nchi hizo pia zitasalia katika mpango wa biashara huria wa umoja huo.Vile vile, mwenyekiti wa AES, mtawala wa kijeshi wa Mali Assimi Goïta, alisema Januari mwaka jana kwamba haki ya raia wa Ecowas "kuingia, kuzunguka, kuishi, kuanzisha na kuondoka katika eneo" la jumuiya hiyo mpya itadumishwa.

Ilyasu Gadu, mtaalamu wa masuala ya kimataifa na mshauri wa vyombo vya habari anayeishi katika mji mkuu wa Nigeria Abuja, aliiambia BBC: "Viongozi hao watatu wamechukua hatua kusema: 'Ndiyo, tunajiondoa Ecowas lakini tunataka kudumisha uhusiano wetu...tusifunge mipaka yetu' kwa sababu lazima wangetambua kwamba kama wangefanya hivyo, ingekuwa sawa na kujidhoofisha."

Waangalizi wa Afrika Magharibi pia wana wasiwasi kujiondoa huko kutaathiri usalama katika eneo hilo. Sahel - eneo lenye ukame kusini mwa Jangwa la Sahara ambalo linajumuisha nchi tatu zinazojiondoa - linakabiliwa na uasi wa jihadi na sasa linachangia "karibu nusu ya vifo vyote vinavyotokana na ugaidi duniani", afisa mkuu wa Umoja wa Mataifa alisema mwezi Aprili.

Ecowas ilikuwa ikiziunga mkono Mali, Burkina Faso na Niger katika vita vyao dhidi ya wanajihadi, lakini msaada huu sasa unaweza kufutwa, waangalizi wanahofia.

Ingawa utawala wa kijeshi sasa unapokea silaha na mamluki kutoka Urusi, wanamgambo hao wanaendelea kuwasababishia hasara kubwa raia na vikosi vya jeshi.Je, uamuzi huu utaathiri vipi Ecowas?Ecowas itapoteza watu milioni 76 kati ya watu wake milioni 446 na zaidi ya nusu ya eneo lake lote la ardhi.

Pia kuna wasiwasi kwamba kujiondoa kutadhoofisha umoja wa kikanda na ushirikiano katika kupambana na uasi.Mgawanyiko huo "unazidisha mgogoro wa uhalali wa ECOWAS ambao mara nyingi umeshindwa kukidhi matarajio ya watu katika kuzingatia utawala wa sheria," Ulf Laessing, mkuu wa mpango wa Sahel katika Wakfu wa Konrad Adenauer, aliiambia Associated Press.

"Kwamba nchi tatu masikini zaidi wanachama ziliamua kuondoka kwenye kambi hiyo inaifanya Ecowas machoni pa raia wake kuonekana kama mtu aliyeshindwa katika mzozo huu."



# RASHFORD

## ANAVYOMCHEFUA KOCHA WAKE

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim amegonga vichwa vya habari aliposema, ni bora kumuweka kama mchezaji wa akiba kocha wake wa makipa mwenye umri wa miaka 63, kuliko Marcus Rashford, kwa sababu hana juhudi.

Rashford hajacheza kwenye kikosi cha United kwa muda wa wiki sita. Amorim anasema mshambuliaji huyo wa Uingereza hafanyi vyema katika mazoezi.

Mustakabali wake ndani ya Old Trafford haujulikani. Kuna klabu za Ulaya zinazohusishwa na kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji wiki ijayo.

Sio mara ya kwanza kwa kocha wa Ligi Kuu England kumkosoa hadharani mmoja wa wachezaji wake.

Harry Redknapp na Darren Bent

Harry Redknapp alidai kuwa mke wake angefunga, pale Darren Bent alipokosa bao dakika za lala salama. Siku Tottenham ilipotoka sare ya 1-1 na Portsmouth Januari 2009.

Redknapp alisema: “Huwezi kupata nafasi nzuri zaidi ya kushinda goli kuliko ile uliyoipata. Hata mke wangu angeweza kufunga.”




Licha ya kauli hiyo, Bent alibaki kwenye safu ya wachezaji wa Redknapp na alimaliza msimu wa 2008-09 kama mfungaji bora wa Tottenham akiwa na mabao 17, kabla ya kujiunga na Sunderland majira ya kiangazi.

Redknapp alitumia miaka mingine mitatu na nusu akiwa White Hart Lane (Tottenham) akiwasaidia kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mwaka 2011, lakini alitimuliwa Juni 2012.

Harry Redknapp na Adel Taarabt

Redknapp, wakati huo akiwa meneja wa QPR, hakusita kumkosoa Adel Taarabt alipoulizwa kwa nini kiungo huyo ameachwa nje ya kikosi kwenye mchezo dhidi ya Liverpool, Oktoba 2014.

“Siwezi kuwalinda watu ambao hawataki kukimbia na kufanya mazoezi, na wana uzito wa mawe matatu,” alisema Redknapp.

“Alicheza katika mchezo wa timu ya kikosi cha pili juzi na ningeweza kukimbia zaidi ya alivyokimbia yeye. Siwezi kumchagua.”

Taarabt ilijibu kwa kusema Redknapp alikuwa akitoa visingizio kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo, wakati huo timu ikiwa nafasi ya chini kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Kiungo huyo aliichezea klabu hiyo mechi tano tu, kabla ya kujiunga na Benfica msimu wa joto wa 2015.

QPR ilishuka daraja mwishoni mwa msimu wa 2014-15. Redknapp aliipandisha tena daraja timu hiyo msimu uliofuata kabla ya kung'atuka Januari 2015.

KUMEKUCHA

MICHEZO

IJUMAA, JANUARI 31, 2025



# Salah anukia Al Hilal

Al-Hilal wamepewa nafasi kubwa ya kumsajili winga wa Liverpool kutoka Misri Mohamed Salah, 32, msimu huu baada ya timu hiyo ya Saudi Pro League kubatilisha mkataba wa mshambuliaji wa Brazil Neymar, 32. (Telegraph – Subscription Required).

# Man Utd wajitosa kwa Casemiro

Roma wanataka kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Brazil Casemiro, 32, kwa mkopo hadi mwisho wa msimu huu, lakini uhamisho unategemea kumuuza mchezaji wa kimataifa wa Argentina Leandro Paredes, 30. (Mail),.

# Samia Suluhu academy kuchochea Utalii

NA MWANDISHI

**WETU,Zanzibar**
**KATIBU wa Itikadi,Uenezi na Mafunzo,Amos Makalla,amesema,kukamilika kwa uwanja wa mpira wa kisasa wa Samia suluhu Academy,utaongeza utalii wa kimichezo Visiwani Zanzibar.**



Makala ameyasema hayo jana wakati wakati wa ziara yake katika Mkoa wa Kusini Unguja na kukagua miradi mbalimbali ya kimkakati akianzia Samia Sport Academy Ujenzi wa Uwanja wa Kisasa utakaochukua Watazamaji 23000.

Alisema,mbali ya kukuza utalii kwa timu zote zitakazokuja Kizimkazi uwanja na chuo hicho utatumika kukuza vipaji vya wanasoka nchini.

Katika ziara hiyo Makalla,alikagua Kituo cha Afya cha Kisasa kiitwacho Kizimkazi Center ambacho kimejengwa kwa gharama Bilioni 7 na kitahudumia Wananchi Elfu 13.

Pia kituo hicho kitasaidia eneo kubwa na Mradi wa Daraja pamoja na kutembelea Skuli ya Elimu Mjumuisho Jendele inayohudumia watoto wenye mahitaji maalumu ndani ya Kusini Unguja.

# Winga mpya Yanga kuanza na Kagera Sugar

**NA MWANDISHI WETU**

**NI kama vile mashabiki wa klabu ya Yanga hawajapata muda mzuri ya kumuangalia na kumfanyia tathmini winga wao mpya Jonathan Ikangalabo, aliyesajiliwa katika kipindi cha dirisha dogo, hivyo wanatamani Jumamosi ifike hata leo ili waweze kumuona nyota wao huyo.**

**Yanga itaumana na Kagera Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC Jumamosi katika uwanja wa KMC, ambapo taarifa zinadokeza kuwa kocha Mkuu wa Yanga Sead Ramovic amepanga kutumia mchezo huo kumjaribu Ikangabo aliyesajiliwa kutoka As Vita ya nchini DRC.**

**Kabla hajajiunga na Yanga winga huyo alikuwa tegemeo akiisaidia sana timu hiyo ya awali ambapo Yanga ilivutika naye baada ya kuona kiwango chake.**

**Inadaiwa Ikangalabo licha ya kucheza nafasi zote za pembeni lakini ni mchezaji mwenye kasi kubwa na uwezo wa kupachika mabao kutokea pembeni, pia ni mtaalamu wa kujipiga kona.**